# IJA - WORKERS SACCOS LTD.

Reg. No. TAR 526, P.O.Box 20, Lushoto – Tanga. Tel:+255 (0) 272660133.

Fax: +255 (0)272660021, E-mail: ijaworkerssaccos@gmail.com


*Kumb. Na. IJAWOSA/CORR./VOL.II/10* **23/5/2019**

*Mrajisi msaidizi,*
*Vyama vya Ushirika Mkoa,*
S.L.P 5095
**TANGA.**

**K.K.** Afisa Ushirika, (W)
S.L.P 22,
**LUSHOTO.**

Imepitishwa
Kwa hatua Zaidi
29/05/2019

AFISA USHIRIKA (W)
LUSHOTO

**YAH: MAOMBI YA KURIDHIA SERA ZA CHAMA CHA IJA WORKERS SACCOS LTD**

Tafadhali husika na somo tajwa kwenye kichwa cha habari hapo juu,

Kwa heshima kubwa ninakutumia nakala tatu (3) za Sera za Chama cha IJAWOSA LTD kwa ajili ya kuzipitia na kisha ukiridhia uzipe kibali chako kwa ajili ya matumizi ya Chama.

Sera hizi zilipata ridhaa na Baraka za Mkutano Mkuu Mikuu ya Kawaida ya Wanachama iliyofanyika tarehe 30/06/2018 na 03/11/2018 ambapo baada ya Wamnachama kuzipokea, kujadili na kuziridhia, walikasimu madaraka kwa Bodi ya Chama kuzifanyia kazi na hatimaye kuziwasilisha kwako kwa hatua za mwisho.

Aidha Sera zilizotumwa kwako ni;

- Sera ya Menejimenti na Majanga;
- Sera ya Mikopo;
- Sera ya Hisa, Akiba na Amana;
- Sera ya Uwekezaji;
- Sera ya Menejimenti ya Ukwasi, Mali na Dhima;
- Sera ya Elimu na Mafunzo;
- Sera ya Fedha na Uhasibu;
- Sera ya Ukaguzi;
- Sera ya Utunzaji kumbukumbu;
- Kanuni za Menejimenti ya Rasilimali Watu na Utawala;
- Kanuni za Maadili kwa Wanachama, viongozi na Watendaji.

Pamoja na salaam za ushirika, ninatanguliza shukrani.

......................

**George J. Banoba**
**MWENYEKITI**

IJA WORKERS SACCOS LIMITED
P. O. BOX 20
LUSHOTO
REG. NO. TAR.526

CamScanner